# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu
Mkuu wa Shule **0757948460/0624709485**
Makamu Mkuu wa Shule **0762513876**

Shule ya Sekondari Iwawa
S.L.P. 33,
**Makete**
**23/05/2018**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..............................**
..........................................................................................
S.L.P. ...............................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IWAWA HALMASHAURI YA MAKETE MKOA NJOMBE MWAKA 2018**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2018 tahasusi/mchepuo wa ............... Shule ya Sekondari Iwawa ipo umbli wa Kilometa112 kutoka Njombe na kilomita 84 kutoka Mbeya Mjini. Wanaotoka Mikoa ya Kagera, Geita, Mara, Mwanza na Shinyanga utapanda mabasi ya moja kwa moja ya Mwanza-Mbeya, ukifika Mbeya kituo kidogo cha mabasi Uyole utapanda mabasi ya Mbeya-Makete (**Japanise Express au Ukinga Ng'aning'ani**). Wanaotokea, Manyara, Arusha na Tanga utapanda mabasi ya moja kwa moja ya Arusha -Mbeya, ukifika Mbeya kituo kidogo cha mabasi Uyole utapanda mabasi ya Mbeya-Makete (**Japanise Express au Ukinga Ng'aning'ani**). Mikoa ya lindi na Mtwara utafika Dar-es-salaam na kupanda mabasi yaendayo Njombe, ukifika Njombe standi utapanda mabasi yaendayo Makete Mjini mabasi hayo ni **Sikinde Express, Mwafrika Bus Service, Penguin na Japanise**. Wanaotokea mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar-es-salaam utapanda mabasi yaendayo Njombe, ukifika Njombe standi utapanda mabasi yaendayo Makete Mjini mabasi hayo ni **Sikinde Express, Mwafrika Bus Service, Penguin na Japanise**. Wanaotoka kanda ya kati na Kigoma utafika Dodoma na kupanda mabasi ya Dodoma- Njombe, ukifika Njombe standi utapanda mabasi yaendayo Makete Mjini. Wanaotokea Iringa utapanda basi la Mwafrika mpaka makete mjini, aidha basi hilo huondoka Iringa saa 12.15 asubuhi.

   Mara ushukapo Makete standi uliza Shule ya sekondari Iwawa (ni Mita 400 tu kutoka standi)

2. Usafiri wa basi kutoka Njombe mjini hadi Makete ni shilingi 10,000/= kutoka Mbeya hadi Makete nauli ni Shilingi 10,000/=

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 02/07/2018.Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuaanzia tarehe 01/07/2018.

3. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**3.1 Sare ya Shule**

a) Suruali Mbili za **rangi damu ya mzee** na **rangi ya mastadi**. (Angalia kiambatanisho **A**-damu ya mzee **B**- Mastadi)

b) Sare ya michezo na Vazi baada ya masomo kwa Shule hii ni Tracksuit nyeusi jozi mbili au zaidi zenye mistari 3 myeupe ya kunyooka.

c) Viatu vya Shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

d) Soksi Nyeusi –Jozi Mbili

e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi

f) Mashati mawili meupe yenye kola – mikono mirefu



g) Sweta Mbili rangi ya bluu

h) T-shirt ya Shule Shilingi 10,000/=

i) Koti zito jeusi lisilo na maandiashi yoyote(makete kuna baridi )

j) Mavazi mengine nje ya sare zilizoagizwa hayaruhusiwi kabisa (asije nayo).

VIAMBATANISHO VYA RANGI ZA SURUALI

| A | B | *NB. Suruali isiwe Modal* |
|---|---|---|
|  |  | • *Miguuni chini iwe na upana wa sentimita kati ya 22-25*<br>• *Ukishona modal hutapokelewa* |

**3.2 Ada na Michango ya Shule**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni Shilingi 70,000.00/=, Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000.00 kwa muhula. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **Namba 60402300136- MFUKO WA TAHADHARI IWAWA SEKONDARI katika Benki ya NMB** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye risiti ya malipo ya benki na fika na risiti hiyo Shuleni)

**b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha

iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

iv) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine

v) Maji na Umeme 7,000/=

vi) Shilingi 10,000/= Matibabu (haitarejeshwa)

vii) Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima(joint exams)

viii) Meza/Dawati 25,000/=

Michango hii ilipwe kwenye akaunti ya shule **Namba ,60401100031-IWAWA SECONDARY SCHOOL, katika Benki ya NMB** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye risiti ya malipo benki, fika na risiti ya benki(Bank Pay Slip) shuleni.

**a) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i) Ream ya karatasi A4 1 (kwa mwaka)
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iii) Godoro kwa wanafunzi wa bweni 2.5x4x6
iv) Mashuka 2 (light blue 1 na pinki 1), blanketi zito1, foronya 1, chandarua 1 (rangi blue)
v) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
vi) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
vii) Kwanja 1 na Mopa au Brash 1 kwaajili ya usafi wa Mabweni na Madarasa.
viii) Picha tatu (3) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

**4. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv) Kutoa **lugha chafu** kwa wanafunzi wenzake, Walimu/Walezi na jamii wa ujumla.
v) **Kupigana** mwanafunzi kwa mwanafunzi, **kumpiga** Mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi) Kufuga ndevu
vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii) Uvutaji wa sigara
ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
x) Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, Siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi.
xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia **simu** ya mkononi. Simu ya shule tu ndiyo itatumika kuwasiliana na Wazazi/Walezi
xv) Kudharau Bendera ya Taifa
xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
xviii) Kutoka nje ya eneo la Shule bila kibali cha Mkuu wa Shule

## KARIBU SANA

Saini ya Mkuu wa Shule; ....[signature]....

Jina la Mkuu wa Shule; FADHILI ELIEZER DONONDA

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IWAWA
S. L. P. 33
MAKETE

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA MAKETE
# SHULE YA SEKONDARI IWAWA

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI.**

**A: AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi.......................................................................Mzazi/Mlezi wa ............................................................ (jina la mtoto) ninakubali mwanangu aje Shule ya Sekondari Iwawa na ninaahidi kumtimizia mahitaji yote yaliyoagizwa. Pia naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule kumlea na kumtunza kwa maadili ya ki–Tanzania (awapo Shuleni na likizoni) mpaka atakapo maliza masomo yake. ***Aidha Sitampa Mwanangu Simu Muda Wote Awapo Shuleni wala mavazi nje ya sare ya shule iliyoagizwa. Mawasiliano yangu yote nitayafanya kupitia Uongozi wa Shule.***

Na kama kuna mabadiliko nitautarifu Uongozi wa Shule.

Anuani yangu ya kudumu: ......................................................................................................................................

Sahihi. .................................................. Tarehe ...................................................

Walezi watakao kuja kumwona mwanafunzi ni;

| | | |
|---|---|---|
| 1.................................................... | 2.................................................... | 3.................................................... |
| bandikapicha | bandikapicha | bandikapicha |

**B: AHADI YA MWANAFUNZI.**

Mimi ............................................................................................ Nakubali/Sikubali* Nafasi niliyopewa katika Shule ya Sekondari ya Iwawa. Naahidi kuwa nitazitii Sheria zote za Shule na kufuata maelezo na maagizo nitakayopewa na Mkuu wa Shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa Serikali ya Wanafunzi.

Nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, elimu ya kujitegemea, michezo na kutunza usafi wa mazingira ya shule kwa muda wote nitakao kuwa Iwawa. ***Aidha sitakuwa na simu muda wote niwapo shuleni wala kuwa na mavazi nje ya sare ya shule niliyoagizwa.***

Shule niliyo soma ni ............................................................ Namba ya Mtihani ni ...........................................................

Sahihi ........................................................ Tarehe ..........................................................

*C: SEHEMU YA MGANGA .*

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## MAKETE DISTRICT COUNCIL

## IWAWA SECONDARY SCHOOL

## (REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IWAWA
S. L. P. 33
MAKETE

This form must be completed by a Government Medical Officer

Name of Student ..........................................................................................................

Age ........................................................... Sex ........................................................

The above named pupil has been examined in respect of

a) PREGNANCY TEST (FOR GIRLS ONLY) ..............................................................
b) STOOL ..........................................................................................................
c) URINE ..........................................................................................................
d) CHEST ..........................................................................................................
e) BLOOD ..........................................................................................................
f) EYES ..........................................................................................................
g) EARS ..........................................................................................................
h) OTHER FINDINGS ...........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

I am satisfied that the above named pupil is fit/not fit for pursuing Secondary studies at IWAWA SECONDARY SCHOOL.

................................................ ........................................

**SIGNATURE** **DATE**

........................................................ ............................................

**DESIGNATION and OFFICIAL STAMP** **STATION**

